

Ripoti Chuki/Ubaguzi

Wanajamii wamefahamisha Washington State Commission on Asian Pacific American Affairs (CAPAA) kuhusu visa vya chuki vinavyolenga watu wa asili ya Asia na Visiwa vya Pasifiki (API) wakati wa janga la COVID-19. Kwa bahati mbaya, CAPAA haifanyi kazi ya jamii, wala hatuwezi kutoa ushauri wa kisheria. Tunawasihi waathiriwa wote wa vitendo vya chuki kuchukua hatua zifuatazo:

Pata usaidizi wa matibabu, ikiwa inahitajika.

Andika maelezo yote ya uhalifu haraka iwezekanavyo baada ya tukio hilo. Jumuisha umri, kimo, rangi, uzani, nguo na sifa zingine za mhalifu (wahalifu) zinazowatofautisha na wengine. Ikiwa vitisho au maoni yoyote ya upendeleo yalifanywa, yajumuishe kwenye ripoti.

Andikisha ripoti. Ripoti tukio hilo kwa watekelezaji sheria katika eneo lako. Ikiwa waathiriwa hawataki kwenda polisi, wasilisha ripoti kwa Jopo Kazi la Haki za Kiraia/Haki za Binadamu katika eneo lako). Hata kama tukio halifikii vigezo vya kisheria vya uhalifu unatokana na chuki, bado ni muhimu kuripoti kwa mamlaka husika. Tafadhali rejelea maelezo yaliyoorodheshwa hapo chini.

Serikali za nchi, kaunti, na mji na mashirika mengine mara nyingi huwa na mahali pa kuripoti vitendo vya chuki na ubaguzi ikiwa ni pamoja na, lakini sio tu, rasilimali zilizoorodheshwa hapo chini:

- [Washington State Human Rights Commission](#)
Chini ya sheria, kila mtu ana haki ya kuwa huru kutokana na ubaguzi kazini, katika makaazi, katika maeneo ya umma, au wakati wa kutafuta mkopo na bima. Mtu yeyote anayeamini kwamba amekuwa akibaguliwa kulingana na hali zilizolindwa za jamii anaweza kufungua mashtaka ya ubaguzi dhidi ya waajiri, watoa huduma za nyumba, na biashara.
- [King County Office of Civil Rights](#)
Ofisi hii ina mamlaka ya kushughulikia malalamiko ya ubaguzi kwa serikali ya Kaunti ya King pekee na kwa waajiri, watoa huduma za nyumba, na biashara katika sehemu ambazo hazijashirikishwa za Kaunti ya King (nje ya miji).
- [Seattle Office for Civil Rights](#)
Ofisi hii inasimamia sheria zinazokuinga dhidi ya unyanyasaji wa kibaguzi katika makazi, ajira, au maeneo ya umma ndani ya mipaka ya jiji la Seattle.
- [Spokane Police Department: Kuripoti Uhalifu Unaotokana Chuki na Upendeleo](#)
Ukurasa huu una maelezo kuhusu ufafanuzi wa uhalifu unaotokana na chuki, na jinsi ya kuuripoti.
- [City of Spokane's Human Rights Commission](#)
Hapa ni pahali sahihi pa kupata usaidizi iwapo wewe ni mwenyeji wa Mji wa Spokane. Ukurasa una maelezo kuhusu malalamiko ya aina tofauti.
- [Fomu ya Kuripoti Tukio la Chuki ya Spokane County Human Rights Task Force](#)
Hapa ndio mahali panapofaa pa kupata usaidizi iwapo unaishi mahali pengine katika Kaunti ya Spokane.

Ripoti tukio hilo kwa mojawapo ya mamlaka zifuatazo ili usaidie katika kuelimisha umma kuhusu mambo yanayotendeka na uchangie katika uundaji wa sera. Unaweza kwenda katika:

- [Simama Dhidi ya Chuki](#)
Asian Americans Advancing Justice inafuatilia matukio ya upendeleo. Kwa kushiriki kile ulichopitia au kushuhudia, unaweza kuelimisha umma, kuwapa wengine nguvu, kuonyesha watoa huduma ambapo usaidizi unahitajika, na kuimarisha juhudi za utetezi katika kukabiliana na kuzuia uhalifu unaotokana na chuki. Fomu zinapatikana kwa lugha za Kiingereza, Kichina (cha jadi na kilichorahisishwa), Kikorea na Kivietinamu.
- [Fomu ya Tukio la Chuki ya AAPI](#)
OCA – Asian Pacific American Advocates imejitolea kuendeleza ustawi wa kijamii, kisiasa, na kiuchumi wa watu wa Waasia Wamarekani na Visiwa vya Pasifiki (AAPI). Kuwasilisha visa vya chuki kupitia fomu hii kutatusaidia OCA – Asian Pacific American Advocates kufuatilia chuki dhidi ya AAPI kote nchini.
- [Komesha Chuki Dhidi ya AAPI](#)
Asian Pacific Policy and Planning Council (A3PCON) na Chinese for Affirmative Action (CAA) wamezindua kituo hiki cha kuripoti ili kuruhusu wanajamii kuripoti matukio ya chuki waliyopitia. Maelezo ya kibinafsi, ikiwa ni pamoja na maelezo ya utambulisho wa kibinafsi, yatahifadhiwa kwa siri na yatashirikiwa tu baada ya idhini kutolewa. Kwa jumla, maelezo yatumika kwa ajili ya usaidizi, utetezi na elimu. Fomu zinapatikana kwa lugha za Kiingereza, Kivietinamu, Kichina, Kikorea, Kikhmer, Kithailandi na Kijapani.

Mwishowe, Human Rights Campaign (HRC) ina mwongozo kwa waathiriwa wa uhalifu unaotokana na chuki: [Nini cha Kufanya Kama Umekuwa Mwachiriwa wa Uhalifu Unaotokana na Chuki](#).